

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



## OFISI YA RAIS

### TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA WAKALA WA MABASI YAENDAYO HARAKA

Kumb Na:AB.23/134/01-G/88

03 Mei 2019

### **TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI**

Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka, Anakaribisha Maombi ya Kazi kutoka kwa watanzania wenye sifa na uwezo wa kujaza nafasi wazi nne (4) kama zilivyobainishwa katika Tangazo Hili.

#### **1. AFISA USALAMA (2)**

##### **1.1. SIFA ZA MUOMBAJI.**

- i. Wahitimu wa kidato cha nne (IV) na sita (VI)
- ii. Awe amehudhuria na kufaulu mafunzo ya Mgambo/Polisi/JKT au mafunzo ya Zimamoto kutoka katika chuo kinachotambuliwa na Serikali.
- iii. Kwa wastaafu wa Jeshi la Polisi, Jeshi la Wananchi wa Tanzania au Jeshi la kujenga Taifa, pamoja na sifa zilizoainishwa katika tangazo hili wanapaswa kuwa na sifa zifuatazo:-
  - hajawahi kushtakiwa kwa kosa lolote la jinai ndani na nje ya kazi alizowahi kuzifanya,
  - Awe na vyeti/cheti/barua ya kustaafu kwake na asiwe alifukuzwa kazi.(Hati ya Utumishi)
  - Awe na umri usiozidi miaka 50.

## **1.2. MAJUKUMU YA KAZI.**

- i. Kulinda usalama wa Majengo, Miundombinu na mali zote zilizopo katika mfumo wa Mabasi Yaendayo Haraka,
- ii. Kufanya ukaguzi na Kutoa taarifa ya hali ya usalama Katika mfumo wa Mabasi Yaendayo Haraka,
- iii. Kusimamia na kuhakikisha kuwa walinzi wa kampuni ya ulinzi iliyopo wanafanya kazi ipasavyo,
- iv. Kusimamia na Kuhakikisha usalama wa abiria na mali zao muda wote wanapokuwa wanapata huduma ya Mabasi Yaendayo Haraka,
- v. Kupambana na Majanga yoyote yanayotokea katika mfumo wa Mabasi Yaendayo Haraka kama vile moto, mafuriko na kutoa taarifa katika vyombo vinavyohusika kama vile polisi na zimamoto,
- vi. Kutoa ushauri jinsi ya kuboresha huduma ya ulinzi mahali pa kazi,
- vii. Kuzuia na kushughulikia matukio yote ya kihalifu yanayotokea katika mfumo wa Mabasi Yaendayo Haraka,
- viii. Kuwa kiungo kati ya jeshi la polisi na Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka,
- ix. Kuandaa taarifa ya kila mwezi kuhusiana na masuala ya ulinzi na usalama katika mfumo,
- x. Kutekeleza majukumu yote kama atakavyokuwa amepangiwa na mkuu wake wakazi.

## **2. TABIBU WA AFYA. (2)**

### **2.1. SIFA ZA MUOMBAJI.**

Wahitimu wa kidato cha nne (IV) au sita (VI) waliofaulu kozi ya Stashahada ya miaka miwili ya utabibu (Up- grading) katika chuo kinachotambuliwa na serikali. Awe na umri kati ya miaka 18 hadi 45.

### **2.2. MAJUKUMU YA KAZI.**

- i. Kutoa huduma za kwanza kwa wagonjwa waliozidiwa katika Mradi wa Mabasi yaendayo Haraka,

- ii. Kuwapeleka kwenye vituo vya afya na hospitali wagonjwa waliozidiwa wakiwa wanapata huduma ya Mabasi Yaendayo Haraka,
- iii. Kutoa elimu na ushauri wa Kiafya kwa abiria wanaotumia huduma ya Mabasi yaendayo Haraka,
- iv. Kuweka kumbukumbu za vifaa na zana za kutolea huduma,
- v. Kuweka kumbukumbu, kuandaa na kutoa taarifa za utekelezaji,
- vi. Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi.

### **3. MASHARTI YA JUMLA KWA KAZI ZOTE.**

- i. Waombaji wote wawe ni Raia wa Tanzania,
- ii. Waombaji wote waambatishe cheti cha kuzaliwa,
- iii. Waombaji waambatishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (Detailed C.V) yenye anwani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini (referees) watatu wa kuaminika.
- iv. Maombi yote yaambatane na vyeti vya kidato cha nne na kidato cha sita, taaluma, kwa wale waliohitimu mafunzo mbalimbali kwa kuzingatia sifa za kazi husika waambatanishe vyeti vya mafunzo husika.
  - i. Testimonials”, “Provisional Results”, “Statement of results”, hati matokeo za kidato cha nne na sita **(FORM IV AND FORM VI RESULTS SLIPS) HAVITAKUBALIWA**
  - ii. Picha moja “Passport size” ya hivi karibuni.
  - iii. Waombaji waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe vyeti vyao vimehakikiwa na Baraza la Mitihani Tanzania – (NECTA).
  - iv. Uwasilishaji wa taarifa na sifa za kugushi wahusika watachukuliwa hatua za kisheria.

**Maombi yote yatumwe kwa:-**

**MTENDAJI MKUU,  
WAKALA WA MBASI YAENDAYO  
HARAKA,  
S.L.P 724,  
DAR ES SALAAM.**

**Mwisho wa kutuma maombi ya kazi ni tarehe 16 Mei 2019.**

Maombi yatakayowasilishwa nje ya utaratibu ulioainishwa katika tangazo hili **HAYATAKUBALIWA.**